IFDC

# I.Habari kuhusu bidhaa

# <u>Mada ya 20a</u>

# Sifa za mbegu

# JARIDA LA UHAKIKA

## I. Habari kuhusu bidhaa

## Mada ya 20a: Sifa za mbegu

Mbegu ni mazao yaliyo hai. Zina sifa, migao na aina mbali mbali. Kwa minajili ya kutumia mbegu vyema tunahitaji kuchagua mbegu vyema, kuchagua mbegu sahihi, tuzipande kwa njia ilio sahihi ili mavuno yawe ya juu.

**Utangulizi kwa sifa za mbegu nzuri**
Mbegu bora zina sifa fulani zinazoweza kutuonyesha matarajio yetu kutoka kwa mbegu hizo. Kabla ya mbegu kuthibitishwa ni lazima zipitie upimaji/uchanganuzi kadha tofauti na ukaguzi shambani. Upimaji/uchanganuzi na ukaguzi huu huonyesha sifa tofauti za kila aina ya mbegu. Sifa muhimu sana za mbegu bora zaweza kufupisha vifuatavyo.

1. Sifa za aina fulani ya mbegu.
2. Sifa za kundi lote la mbegu.

**1. Sifa za aina fulani ya mbegu**
Sifa hizi zinahusu aina za mbegu kwa jumla na zinaweza kugawanywa katika sehemu mbili.

**a. Vipengele vitokanavyo kwa mbegu**

Vipengele vitokanavyo kwa mbegu vinahusu nambari: urefu wa mbegu, umbo la mbegu na uzito wa mbegu elfu moja.

- **Urefu** wa mbegu: Kila aina ya mbegu iliothibitishwa ina urefu uliochapishwa. urefu tofauti ni refu zaidi, refu, refu kadiri, na fupi.
- **Umbo** la mbegu: Kila aina ya mbegu iliothibitishwa ina umbo lililochapishwa: embamba, kadiri, mbegu nzito na mviringo.
- Kila aina ya mbegu iliothibitishwa ina **uzito** wa mbegu elfu uliochapishwa.

**b. Vipengele vitokanavyo kwa mmea**

Kila mbegu iliothibitishwa ina sifa zilizochapishwa zinazoambatana na aina hiyo ya mbegu. Mkulima apandaye mbegu zilizothibitishwa atakuwa na dhana ya jumla kuhusu vile mimea itakuwa/itaonekana na kiwango ambacho mimea hiyo itakua. Hizi sifa ni pamoja na:

- Urefu wa mmea uliokomaa
- Muda kutoka kuota hadi kukomaa
- Rangi ya mmea
- Umbo la mmea

**2. Sifa za kundi lote la mbegu**


Sifa za kundi lote la mbegu zinahusu hali, usafi na uwezo wa kumea wa kundi fulani la mbegu.  Sifa hii inajumuisha yafuatayo:

- Kiwango cha **uchafu**: Uchafu ni kama idadi ya mbegu ya magugu, mbegu za mimea mingine na vitu vitepetevu kama changarawe.
- **Kiwango cha unyevu**: Asilimia ya unyevu katika mbegu huathiri sana muda wa maisha ya mbegu. Kiwango cha juu sana cha unyevu huharibu mbegu.
- **Asilimia ya mbegu zitakazo ota**: Katika kundi la mbegu, kuna mbegu zilizo hai (zitaota zikipata hali inayofaa) na zilizokufa (haziwezi kuota kabisa). Mbegu zilizo hai hupimwa kama asimilia ya mbegu zote kwa jumla. Asimilia ya juu ya kuota inaonyesha mbegu zina uwezo wa matokeo/mazao mazuri shambani

**Kwa nini hizi sifa za mbegu ni muhimu sana?**

Sifa za mbegu huelezea mkulima anachotarajia kama mavuno/mazao ya mimea, idadi ya mbegu itakayoota, kuwepo kwa mbegu za magugu katika mbegu za mazao na vile mimea itakua. Habari hii itamsadia mkulima kupanga vyema na kuendesha kazi ya ukulima kwa njia inayofaa.

Kwa bahati mbaya, sifa hizi zinahusika tu na mbegu zilizothibitishwa/halali. Sifa za mbegu zilizohifadhiwa hazijulikani. Katika hali hii, mkulima hupanda halafu hungojea kuona sifa za mbegu.



# MAELEZO YA ZIADA

## I. Habari kuhusu bidhaa

## Mada ya 20a: Sifa za mbegu

**Urefu wa mbegu**
Kila mbegu zilizothibitishwa/halali zina urefu uliochapishwa

| Maelezo : | Urefu katika milimeta (mm): |
|---|---|
| Refu zaidi | Zaidi ya 7.5 |
| Refu | Kati ya 6.6 na 7.5 |
| Refu kadiri | Kati ya 5.1 na 6.6 |
| Fupi | Chini ya 5.1 |

**Umbo la mbegu**
Kila mbegu zilizothibitishwa/halali zina uwiano wa urefu na upana uliochapishwa

| Maelezo: | Urefu katika milimeta (mm): |
|---|---|
| Embamba | Zaidi ya 3 |
| Kadiri | Kati ya 2.1 na 3 |
| Mbegu nzito | Kati ya 1.1 na 2 |
| Mviringo | Chini ya 1.1 |

# MWONGOZO

## I. Habari kuhusu bidhaa

## <u>Mada ya 20a:</u> Sifa za mbegu

### Vifaa vinavyohitajika:

- ☑ Ubao ulio na makaratasi
- ☑ Markers (1 nyeusi, 1 bluu, 1 kijani, 1 nyekundu)
- ☑ Kadi za rangi
- ☑ Ukanda wa kubandikia

### Muda unaohitajika: Dakiki 60

### Maandalizi:

- ☑ Karatasi ya kufungua kurasa yalio na kichwa: *Sifa za mbegu*
- ☑ Kundi la kadi za rangi zilizo na maandishi/maneno yafuatayo:
  - *Urefu wa mbegu*
  - *Umbo la mbegu*
  - *Uzito wa mbegu elfu moja*
  - *Urefu wa mmea uliokomaa*
  - *Muda kati ya kuota kwa mbegu na kukomaa kwa mmea*
  - *Rangi ya mmea*
  - *Umbo la mmea*
  - *Uchafu katika mbegu*
  - *Kiwango cha unyevu*
  - *Uwezo wa kuota*
- ☑ Karatasi ya kufungua kurasa ilio na mchoro wa mbegu ambao umeandikwa neno mbegu juu ya karatasi.
- ☑ Kadi za rangi zilizo na maneno/maandishi yafuatayo:
  - *Vipengele vitokanavyo kwa mbegu*
  - *Vipengele vitokanavyo kwa mmea*

# Mwanzo

| | |
|---|---|
| **U**sikivu: | Uliza washiriki: Ukiomba kazi mpya, mwajiri hutaka maelezo binafsi ya mtu kabla ya mahojiano. Kwa nini? Watajibu ya kwamba kabla ya mwajiri akuandike kazi anataka ajue wewe ni nani, unaweza kufanya kazi gani na anachotarajia kutoka kwako. Kubaliana nao. |
| **K**ichwa: | Ambia washiriki kichwa huku ukiwaonyesha karatasi ya kufungua kurasa ilio na kichwa: *Sifa za mbegu.* |
| **K**usadikika: | Elezea uzoefu wako katika uwanja wa mbegu |
| **M**alengo: | Kuelezea sifa mbalimbali/tofauti za mbegu. |
| **M**anufaa: | Kuelewa sifa za mbegu kutakusaidia kutofautisha kati ya mbegu zilizo za ubora wa juu na mbegu duni. |
| **M**welekeo: | Katika kipindi hiki, tutaangazia sifa mbalimbali za mbegu kwa jumla. Hatutajadili uchanganuzi wa sifa hizo. |

# Wasilisho

## **U**fafanuzi, **M**aonyesho, **M**azoezi, na **M**wongozo:

1. Waambie washiriki kwamba mbegu, hususa mbegu zilizothibitishwa/halali pia zina maelezo binafsi kama mtu atafutaye kazi. Maelezo ya binafsi ya mbegu ndio **sifa** za mbegu. Sifa hizi zitatuambia aina ya mbegu, zinayoweza kuyafanya mbegu hizi na tutakachotarajia kutoka kwa mbegu hizo.
2. Uliza washiriki kutaja sehemu kuu za mahojiano ya kazi. Waongoze wafikie majibu haya:
    - Habari zote za kibinafsi na asili ya mhojiwa
    - Ustahilifu
    - Ujuzi na marifaa
3. Waambie kwamba tunahitaji kujua habari kama hiyo juu ya mbegu kabla ya kuamua ni mbegu gani tutapanda.
4. Gawanya washiriki katika vikundi vya watu wawili au watatu. Bandika karatasi ya kufungua kurasa yenye mchoro wa mbegu kwa ukuta. Waambie washiriki kwamba mbegu hiyo imeomba kazi ya mbegu iliothibitishwa/halali na tutaendesha **mahojiano ya mbegu** kuangalia kwa kweli kama mbegu hiyo ni mbegu iliothibitishwa/halali. Kila kikundi kitayarishe maswali kuamua tunachotarajia kutoka kwa mbegu na mmea (sifa). Kwa mfano, mmea uliokomaa utakuwa na urefu gain? Washiriki waandike maswali yao katika daftari zao. Wape dakika chache za kujadiliana.
5. Jadili majibu. Itisha **swali** moja kutoka kwa kikundi cha kwanza. Kama swali hilo linalingana na yale yalioko kwenye kadi za rangi za sifa, chukua kadi hiyo

inayolingana na swali na urudie swali hilo ukionyesha kadi hiyo kwa washiriki wote. Kwa mfano, kama swali ni “mmea uliokomaa utakuwa na urefu gani?”, chukua kadi ilioandikwa “Urefu mmea uliokomaa”, elezea kadi hiyo kwa kina halafu uibandike kwenye ukuta.

Ukumbusho: Hakutakuwa na makundi yoyote ukutani kwa wakati huo. Bandika kadi zote zinazoingia chini ya kundi la vipengele vitokanavyo kwa mbegu katika upande wa kushoto wa ukuta, zile za vipengele vitokanavyo kwa mmea katikati mwa ukuta na zile za sifa za kundi lote la mbegu katika upande wa kulia wa ukuta.

6. Uliza kikundi cha pili swali lao halafu urudie hatua zile. Rudia mpaka wakati ambapo kila kikundi kitakuwa kimetoa mawazo yao.
7. Mwishowe, kadi zote za rangi za sifa ziwe kwenye ukuta. Kama kuna kadi ambazo hazijatajwa, elezea sifa hizo halafu ubandike kadi hizo kwenye ukuta. Kadi zigawanywe kwenye vikundi vitatu: Vipengele vitokanavyo kwa mbegu, vitokanavyo kwa mmea na za kundi lote la mbegu.
8. Kadi zote za sifa zikishabandikwa ukutani, ongeza vichwa vya kila kikundi: *Vipengele vitokanavyo kwa mbegu, vipengele vitokanavyo kwa mmea na vipengele vitokanavyo kwa kundi lote la mbegu.* Matokeo yatakiwa yawe ifuatavyo:
    a. **Vipengele vitokanavyo kwa mbegu**: Urefu wa mbegu, umbo la mbegu, na uzito wa mbegu elfu moja
    b. **Vipengele vitokanavyo kwa mmea**: Urefu wa mmea uliokomaa, muda kati ya kuota hadi kukomaa kwa mmea, rangi ya mmea, na umbo la mmea.
    c. **Sifa za kundi lote la mbegu**: kiwango cha uchafu, kiwango cha unyevu, na asilimia ya mbegu zitakazo ota
9. Uliza swali: **Kwa nini sifa hizi ni muhimu sana**? Ongoza majibu kwa: Hizi sifa zinatusaidia kutofautisha kati ya mbegu zilizo na ubora wa juu na zile zilizo duni.

# Malizia

**M**uhtasari: Peana muhtasari kwa kuwambia washiriki kwamba mbegu zina sifa fulani. Baadhi ya hizi sifa zinahusika na aina za mbegu, ukuzaji wa mmea na hali inayofaa kwa kundi la mbegu fulani. Kariri sifa kuu ukitumia kadi zilizo kwenye ukuta.

**M**aswali: Uliza kama kuna yeyote aliye na swali au maoni.

**T**athmini**:** Uliza washiriki kutaja makundi matatu ya sifa za mbegu. Uliza sifa za vipengele vitokanavyo kwa mbegu, kwa mmea au kwa kundi lote la mbegu. Uliza kwa nini sifa hizi ni muhimu kuzijua.

**H**atua fuatilizi: Katika kipindi hiki, tumejifunza kuhusu sifa za mbegu bora. Katika somo lifuatalo, tutajifunza jinsi ya kutambua baadhi ya sifa hizi kwa kutumia kip rahisi.

Sambaza **makaratasi ya taarifa ya maelezo** kwa washiriki wote.